# TUME YA VYUO VIKUU TANZANIA (TCU)

# TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

## MAFANIKIO YA TUME YA VYUO VIKUU TANZANIA (TCU) KATIKA KIPINDI CHA UONGOZI WA SERIKALI YA AWAMU YA TANO

### 1.0 UTANGULIZI

**Ndugu Waandishi wa Habari,**

Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuweka hai, kutujalia nguvu na afya ya kutekelekeza kwa ufanisi majukumu yetu ya kuwatumikia Watanzania.

Pili, napenda kuwatakia kheri ya Mwaka Mpya 2020 na nichukue fursa hii kuwakaribisha katika Ofisi zetu za Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU) zilizopo katika Jengo la Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Mtaa wa Magogoni.

Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania tunaamini kuwa ninyi ni wadau muhimu katika mchakato wa maendeleo kwani kupitia kwenu, taarifa mbalimbali zinazohusu Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania zinawafikia umma wa Watanzania.

Leo **Januari 28, 2020** nitaelezea mafanikio ya Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania yaliyopatikana katika kipindi cha uongozi wa Serikali ya Awamu ya Tano. Tathmini yetu imejikita katika kipindi cha kuanzia Novemba 2015 hadi sasa.

**Ndugu Waandishi wa Habari,**

Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU) ni Taasisi ya Serikali, iliundwa mwaka 2005 kwa Sheria ya Vyuo Vikuu, Sura ya 346 ya Sheria za Tanzania. TCU ilitokana na

maboresho yaliyofanywa na Serikali kwa lililokuwa Baraza la Ithibati la Elimu ya Juu (HEAC) lililoanzishwa mwaka 1995 kwa Sheria ya Elimu Sura ya 523 ya Sheria za Tanzania.

Lengo la kuanzishwa HEAC ilikuwa kuthibiti ubora wa vyuo vikuu nchini vilivyokuwa vinaanzishwa na kuendeshwa na taasisi binafsi. Uanzishwaji wa vyuo binafsi ulitokana na mabadiliko yaliyofanywa na serikali katika uendeshaji wa elimu ya juu mwishoni mwa miaka ya 1980 na mwanzoni mwa miaka ya 1990 (liberisation of higher education). Ili kuweka mahusiano mazuri kati ya serikali na sekta binafsi (Public Private Partnership) na uoanishaji wa elimu itolewayo na vyuo vikuu nchini, pamoja na kuzingatia kuwa suala la ubora ni mtambuka linahusu taasisi zote zinazotoa elimu ziwe taasisi za serikali au taasisi binafsi, Baraza lilifanyiwa maboresho na mwaka 2005 iliundwa Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU) ambayo iliongezewa majukumu ikiwa ni pamoja na kuthibiti ubora katika vyuo vikuu vinavyomilikiwa na kuendeshwa na Serikali.

TCU ilipewa majukumu makubwa matatu: Kwanza, ni kusimamia sheria, kanuni na taratibu za uanzishaji na uendeshaji wa vyuo vikuu nchini. Pili, kusaidia na kutoa miongozo kwa vyuo vikuu kuhusu uthibiti wa ubora wa vyuo vikuu, njia mbalimbali za uendeshaji wa vyuo, kuandaa na kuratibu mafunzo mbalimbali kwa Wahadhiri, waendashaji na viongozi wa vyuo vikuu nchini. Jukumu la tatu ni kutoa ushauri kwa umma, vyuo vikuu, na serikali kupitia waziri mwenye dhamana ya elimu nchini kuhusiana na mabadiliko mbalimbali ya sayansi, teknolojia, sera na muelekeo wa elimu ya vyuo vikuu nchini na duniani kwa ujumla.

Dira ya TCU ni kuwa taasisi inayoongoza kikanda katika kusimamia ukuaji na maendeleo endelevu ya elimu ya vyuo vikuu nchini. Dira hii inatekelezwa kupitia dhamira ya TCU ya kuhakikisha uwepo wa mifumo endelevu ya elimu ya ngazi ya chuo kikuu ili kupata wahitimu wenye elimu, maarifa, ujuzi na uwezo wa kustahimili ushindani kitaifa, kikanda na kimataifa.

## 2.0 MAFANIKIO KATIKA KIPINDI CHA MIAKA MINNE

Katika uongozi wa Serikali ya Awamu ya Tano, TCU imetekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa kama yalivyoainishwa katika Sheria ya Vyuo Vikuu, Sura 346 ya Sheria za Tanzania. Mafanikio haya yanaonesha jinsi serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ilivyoiwezesha TCU kuweza kutekeleza majukumu yake kama yalivyo matakwa ya sheria. Baadhi ya mafanikio hayo ni yafuatayo:

**Kuthibiti ubora wa elimu inayotolewa na vyuo vikuu**

TCU imeendelea kuimarisha mifumo yake ya uthibiti ubora ili kuhakikisha inatimiza jukumu lake la kuhakikisha vyuo vikuu vinaendana na mwelekeo wa nchi, ambao Tanzania imelenga kuwa Taifa la watu wenye maarifa, ujuzi mkubwa, weledi na uwezo wa kutatua changamoto za kijamii na kiuchumi kwa manufaa ya wananchi wake ifikapo mwaka 2025 pamoja na kuifanya Tanzania kuwa nchi ya uchumi wa kati unaochochewa na uwepo wa viwanda.

Kwa mara ya kwanza tangu TCU ianzishwe imefanya ukaguzi maalum wa kitaaluma kati ya Oktoba 2016 na Januari 2017 kwa taasisi zote 64 za vyuo vikuu, vyuo vikuu vishiriki, na vituo vya vyuo vikuu. Lengo la ukaguzi huo lilikuwa kuhakikisha kuwa elimu ya juu itolewayo inakidhi viwango vya kitaifa, kikanda na kimataifa. Matokeo ya ukaguzi yalibainisha kasoro mbalimbali katika uendeshaji wa vyuo vikuu nchini. Vyuo 45 vilikutwa na kasoro ndogondogo, vilipewa ushauri na viliweza kurekebisha katika kipindi kifupi vikaendelea na utoaji wa elimu ya juu. Vyuo 19 vilikutwa na kasoro kubwa, vilipewa ushauri na muda wa marekebisho. Hata hivyo havikuweza kurekebisha katika kipindi kifupi na hivyo kuzuiwa kudahili wanafunzi wapya kuanzia mwaka wa masomo 2017/2018 na viliendelea kupewa ushauri na muda zaidi kufanya maboresho.

Hadi sasa, vyuo vikuu tisa (9) kati ya 19 vilivyositishwa udahili vimefanya marekebisho makubwa na vimeruhusiwa kudahili na kuendelea kutoa mafunzo kwa baadhi ya programu za masomo. Vyuo hivyo ni pamoja na Chuo Kikuu cha Umoja wa Afrika Tanzania (UAUT); Chuo Kikuu cha Teofilo Kisanji (TEKU); Chuo Kikuu Kishiriki cha Askofu Mkuu Mihayo - Tabora (AMUCTA); Chuo Kikuu cha Kimataifa cha Kampala nchini Tanzania (KIUT); Chuo Kikuu Kishiriki cha Marian (MARUCo); Chuo Kikuu Kishiriki cha Uhandisi na Teknolojia cha Mt. Yosefu (SJUCET); Chuo Kikuu Kishiriki cha Kikristo cha Tiba Kilimanjaro (KCMUCo); Chuo Kikuu Kishiriki cha Kumbukumbu ya Stefano - Moshi (SMMUCo) na Chuo Kikuu Kishiriki cha Afya na Sayansi Shirikishi cha Mt. Fransisko (SFUCHAS).

Kimsingi, mifumo ya ukaguzi na ufuatiliaji wa mara kwa mara imefanya vyuo kufanya maboresho makubwa katika miundombinu ya kufundishia na kujifunzia ikiwa ni pamoja na ujenzi wa maabara za kisasa, mifumo ya mawasiliano ya kielektroniki, madarasa na kuongeza idadi ya viongozi na wahadhiri wenye sifa stahiki kwa mujibu wa sheria, kanuni na miongozo iliyopo.

Hata hivyo, licha ya TCU kutoa ushauri, mafunzo na namna mbalimbali za uboreshaji, pamoja na muda wa kufanya maboresho, baadhi ya vyuo havikufanikiwa kufanya maboresho kama inavyotakiwa. Kwa kuzingatia muda uliotolewa na hali ya vyuo husika ikiwa ni pamoja na changamoto ya uhaba wa rasilimali watu na fedha, ilibainika kuwa baadhi ya vyuo havina uwezo wa kujiendesha hata vikipewa muda zaidi, hivyo Tume ililazimika kufuta usajili wa vyuo saba (7) na kuelekeza wanafunzi wahamishiwe kwenye vyuo vingine

vinavyokidhi viwango vya ubora. Vyuo vilivyofutwa usajili ni Chuo Kikuu cha Eckenforde Tanga (ETU); Chuo Kikuu cha Kimataifa cha Tiba na Teknolojia (IMTU); Chuo Kikuu cha Mlima Meru (MMU); Chuo Kikuu cha Tumaini - Kituo cha Mbeya (TUMA - Mbeya Centre); Chuo Kikuu cha Teofilo Kisanji - Kituo cha Tabora (TEKU - Tabora Centre); Chuo Kikuu cha Josiah Kibira (JoKUCo) na Chuo Kikuu cha Bagamoyo (UoB). Aidha, jumla ya wanafunzi 2,607 wa fani za sayansi ya elimu, Sanaa ya elimu, Sanaa ya rasilimali watu, Elimu maalum na Udaktari wa binadamu walihamishiwa katika vyuo vingine.

**Kuimarika kwa mifumo ya vyuo vikuu ya uthibiti ubora**

Kufuatia makongamano na semina elekezi zilizoandaliwa na kuratibiwa na TCU kwa viongozi, wahadhiri na wafanyakazi waendeshaji wa vyuo vikuu zenye lengo la kubadilishana uzoefu, tafsiri ya miongozo mbalimbali na maendeleo ya elimu ya vyuo vikuu duniani, vyuo vikuu vimeweza kuimarisha mifumo yake ya uthibithi ubora na uendeshaji wa mafunzo. Matokeo ya makongamano hayo ni pamoja na tathmini binafsi zilizofanywa na vyuo vyenyewe. Kufuatia tathmini hizo baadhi ya vyuo vimeiomba Tume kusitisha uendeshaji ili viweze kujipanga upya. Taasisi ambazo Tume imesharidhia maombi yao na kufuta usajili wake ni pamoja na; Chuo Kikuu cha Jomo Kenyatta cha Kilimo na Teknolojia - Kituo cha Arusha (JKUAT - Arusha Centre); Chuo Kikuu cha Mt. Yohana - Kituo cha Msalato (SJUT - Msalato Centre); Chuo Kikuu cha Kenyatta - Kituo cha Arusha (KU - Arusha Centre); Chuo Kikuu cha Mt. Yohana cha Tanzania - Kituo cha Mt. Marko (SJUT - Mt. Marko Centre); Chuo Kikuu Kishiriki cha Askofu Mkuu Yakobo (AJUCo); Chuo Kikuu Kishiriki cha Kumbukumbu ya Kadinari Rugambwa (CARUMUCo) na Chuo Kikuu cha Teofilo Kisanji - Kituo cha Dar es Salaam (TEKU - Dar es Salaam Centre). Vilevile zipo programu 33 za masomo kutoka katika vyuo vinavyoendelea na mafunzo ambazo nazo zimesimamishwa kwa muda kufuatia maombi ya vyuo husika.

**Kuwezesha vyuo vikuu katika masuala mbalimbali ya uendeshaji**

Katika kutekeleza jukumu lake la kuratibu na kuvijengea uwezo vyuo vikuu, TCU kwa kipindi husika imeandaa na kuendesha mafunzo mbalimbali yanayolenga kuboresha elimu ya vyuo vikuu nchini. Mpaka kufikia Novemba 2019, jumla ya wafanyakazi 1,581 kutoka vyuo vikuu vinavyomilikiwa na serikali na taasisi binafsi wameshanufaika na mafunzo hayo. Mada za mafunzo zilihusu uongozi katika vyuo vikuu, utengenezaji mitaala inayoendana na soko, mbinu za ufundishaji kwa wahadhiri ambao hawakusoma fani za ualimu, utengenezaji na utumiaji wa mifumo ya kompyuta, tafsiri ya sifa za kujiunga na vyuo vya elimu ya juu, ulinganifu wa programu (programme benchmarks) na uthibiti ubora. Mafunzo hayo yalilipiwa na serikali kwa asilimia 100.

TCU imerejesha kwa asilimia 100 jukumu la udahili kwa Taasisi za Elimu ya Juu kama yalivyo matakwa ya sheria. Hili limewezekana kwa kutengenezwa mfumo

wa pamoja wa kielekroniki kwa ajili ya kuratibu udahili wa shahada za kwanza kwa vyuo vyote vya elimu ya juu. Mfumo huu umeunganishwa moja kwa moja na mifumo ya vyuo vya elimu juu na umetoa mamlaka kamili kwa vyuo vya elimu ya juu kushiriki moja kwa moja katika udahili wa wanafunzi kupitia seneti zao kama yalivyo matakwa ya sheria. Pia umeongeza uhuru kwa waombaji kuchagua vyuo na programu wanazozipenda. Vilevile umeunganishwa na kanzidata za Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA), Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE), Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) na Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu Zanzibar (ZHELB). Uunganishwaji huu umerahisisha upatikanaji wa taarifa za udahili wa wanafunzi wa elimu ya juu na kuiwezesha TCU kuhakiki sifa za wanafunzi wanaodahiliwa na vyuo vya elimu ya juu kwa uhakika na ufanisi zaidi na pia umerahisisha upatikanaji wa taarifa za wanafunzi kwa taasisi za mikopo ya elimu ya juu.

## Kuwekeza katika mitaala ya programu za vipaumbele vya kitaifa

TCU imeendelea kushauri vyuo vikuu kuandaa mitaala inayoendana na vipaumbele vya maendeleo ya taifa, mahitaji ya soko la kitaifa, kikanda na kimataifa pamoja na maendeleo ya sayansi na teknolojia ikiwamo mapinduzi ya nne ya viwanda. Baadhi ya vyuo vikuu vimeshatengeneza na kuanza kufundisha mitaala ya aina hiyo, kwa mfano Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela (NM-AIST); Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA); Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUHAS); Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST) na Chuo Kikuu cha Kikatoliki cha Afya na Sayansi Shirikishi (CUHAS). Baadhi ya mitaala hiyo ni ya programu za Embedded and Mobile Systems, Information Systems and Network Security, Wireless and Mobile Communication, Food Science and Technology, Sustainable Agriculture, Biodiversity and Ecosystem Management, Health Molecular Biology, Animal Reproduction and Biotechnology, Biotechnology and Laboratory Sciences, Plastic and Reconstructive Surgery, Interventional Radiology, Neuroradiology, Medical Imaging and Radiotherapy, Clinical Microbiology and Diagnostic Molecular Biology, Data Science, Cyber Security and Digital Forensic na Digital Instructional Design.

## Elimu kwa umma

Mifumo ya utoaji wa elimu kwa umma imeimarika na wadau wengi zaidi wamefikiwa ndani na nje ya nchi kupitia Maonesho ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia yanayofanyika kila mwaka, redio, televisheni, magazeti, tovuti, mitandao ya kijamii na programu maalumu za kuwatembelea wanafunzi mashuleni na katika makambi ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT). Jumla ya wahitimu 19,196 wa kidato cha sita waliokuwa katika makambi 17 ya JKT na wanafunzi takribani 12,000 waliokuwa kidato cha tano na sita kutoka Unguja na Pemba wamenufaika na programu hii ya elimu kwa umma mwaka 2019. Aidha, idadi ya

taasisi zinazoshiriki Maonesho ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia imeongezeka kutoka 60 mwaka 2016 hadi 87 mwaka 2019. Idadi ya wananchi wanaotembelea maonesho nayo imeongezeka kutoka 20,000 mwaka 2018 hadi 30,000 mwaka 2019. Hamasa ya wananchi imeongezeka hasa baada ya vyuo kuweka madawati ya udahili katika maonesho.

Kuogezeka kwa uelewa wa wananchi kuhusu majukumu ya TCU na taratibu za udahili katika vyuo vya elimu ya juu kumepunguza kwa kiasi kikubwa changamoto za udahili wa elimu ya juu katika kipindi hiki ikilinganishwa na miaka iliyopita. Aidha, takwimu zinaonesha kuwa idadi ya wadahiliwa wa shahada ya kwanza katika vyuo vya elimu ya juu imeongezeka kutoka 65,064 mwaka 2015/2016 hadi 87,813 kufikia mwaka 2019/2020 sawa na ongezeko la asilimia 35.

**Kuimarika kwa mifumo ya kielektroniki**

TCU imeimarisha mifumo yake ya kielektroniki ambayo imeongeza tija na ufanisi katika utendaji kazi kwa kuboresha huduma inazotoa kwa wateja na wadau wake kama ilivyoainishwa katika Mkataba wa Huduma kwa Mteja.

Kwa mfano, Mfumo wa kutathmini uhalali wa vyeti vya wahitimu waliotunukiwa tuzo zao na vyuo vilivyo nje ya Tanzania (Foreign Awards Assesment System - FAAS) umeiwezesha Tume kufanya uhakiki na utambuzi wa vyeti kwa muda mfupi kutoka siku 14 za awali hadi siku tatu. Hivyo katika kipindi hiki zaidi ya vyeti 8,328 vimehakikiwa na kufanyiwa utambuzi.

Pia mfumo wa TCU wa kutoa hati ya kutokuwa na pingamizi kwa wananchi wanaotaka kwenda kusoma elimu ya juu nje ya nchi (No Objection Certificate - NOC) umeimarishwa na kuweza kutoa hati ndani ya siku tatu badala ya siku 14. Mfumo huu ni muhimu kwani unawapa fursa wananchi kufahamu uhalali wa vyuo na programu wanazokwenda kusoma, hivyo kuwaepusha na hasara ya kupoteza rasilimali fedha na muda kwa kusoma katika vyuo visivyotambulika. Katika kipindi hiki, zaidi ya maombi 1,077 ya hati ya kutokuwa na pingamizi kwa wanaotaka kwenda kusoma elimu ya juu nje ya nchi, yamewasilishwa TCU na kushughulikiwa.

Aidha, mfumo wa kielektroniki wa kupokea na kuchakata mitaala ya vyuo vikuu ili kuipa ithibati (Programme Management System - PMS) umeimarishwa kwa kuongeza mawasiliano kati ya vyuo na Tume ikiwa ni pamoja na kuelekeza namna ya uandaaji wa mitaala na hatua mbalimbali za mitaala mara baada ya kuiwasilisha TCU na jinsi inavyoshughulikiwa mpaka kupewa ithibati. Hii imeiwezesha Tume na vyuo kutambua mitaala iliyowasilishwa, inayofanyiwa maboresho, iliyorejeshwa vyuoni, iliyo katika hatua za ithibati na iliyopewa ithibati. Katika kipindi hiki cha miaka minne, zaidi ya mitaala 650 imeshughulikiwa.

Vilevile, TCU imeimarisha mfumo wake wa kielektroniki wa kuchakata na kuhifadhi taarifa za vyuo vikuu nchini (Universities Information Management System - UIMS) kwa kuunganisha na mifumo ya udahili ya vyuo vya elimu ya juu nchini. Hivyo kurahisisha upatikanaji wa taarifa za wanafunzi waliodahiliwa, wanaoendelea na masomo pamoja na wahadhiri, wafanyakazi na waendeshaji wa vyuo vikuu nchini. Mfumo huu umewezesha uandaaji wa kitabu cha takwimu kinachoonesha taarifa za vyuo vikuu katika kipindi cha miaka mitano (State of University Education in Tanzania, 2018) ambacho kimetoka kwa mara ya kwanza mwaka 2019. Uandaaji wa kitabu hiki utakuwa endelevu.

**Kusajili Wakala wanaodahili wanafunzi wanaokwenda kusoma vyuo vilivyo nje ya Tanzania**

Kwa takribani miaka zaidi ya 12 zimekuwepo Wakala zinazodahili wanafunzi wanaotaka kusoma elimu ya juu nje ya Tanzania (Overseas Students Recruitment Agencies). Pamoja na kuwa jukumu mojawapo la TCU ni kuzisajili Wakala hizi, utekelezaji wake haukuwahi kufanyika. Sababu mojawapo ikiwa ni kukosekana kwa miongozo ya namna bora ya kuzitambua na taratibu za uendeshaji. Ni katika kipindi hiki cha miaka minne, TCU imeweza kuandaa miongozo ya uanzishwaji na uendeshaji wa Wakala za kudahili wanafunzi wanaotaka kusoma vyuo vilivyopo nje ya nchi. Muongozo huu unajulikana kama "Principles and Guidelines for Licensing Overseas Students Recruitment Agencies and Issuance of a No Objection Certificate".

Kufuatia muongozo huo, TCU imeweza kusajili Wakala tatu (3) zilizokidhi viwango. Wakala zingine tatu ambazo ziliomba kusajiliwa hazikuweza kukidhi sifa stahiki. Wakala zilizosajiliwa ni ***Global Education Link Ltd*, *DARWIN Education Agency Ltd*** na ***Yuhoma Educational Ltd.*** Wakala hizi zitatakiwa kuhuisha usajili wake kila baada ya miaka mitatu. Pia katika mwezi huu wa Januari, 2020, TCU imepokea maombi ya Wakala wengine saba (7) na taratibu za usajili zinaendelea.

Wakala wote ambao hawajasajiliwa wanahimizwa kutuma maombi yao TCU na kukamilisha taratibu za usajili kwa wakati. Ifahamike kuwa kuendesha Wakala wa kudahili wanafunzi wanaokwenda kusoma elimu ya juu nje ya nchi, bila usajili ni kinyume cha Kanuni ya 47 (1) (d) na (f) ya Kanuni za Vyuo Vikuu za mwaka 2013. Wananchi wote wanahimizwa kutumia Wakala wanaotambuliwa na TCU.

## 3.0 HITIMISHO

TCU imeendelea kuandaa makongamano mbalimbali kwa viongozi wa vyuo vikuu ili kubadilishana uzoefu. Vile vile imeendelea kuandaa mafunzo na semina kwa wahadhiri na wafanyakazi waendeshaji wa vyuo vikuu katika maeneo

mbalimbali yanayohusu elimu ya juu na kuhakikisha mitaala ya vyuo vikuu inahuishwa kwa wakati ili kuandaa wahitimu wanaokidhi mahitaji ya kitaifa, kikanda na kimataifa. TCU pia inaendelea kutoa ushauri kwa vyuo kuweka mikakati ya kuhusisha sekta binafsi na viwanda katika utoaji wa mafunzo na kufanya tafiti ili kujenga ubia na uhusiano wa karibu baina ya sekta binafsi, viwanda na vyuo vikuu. Aidha, TCU imeendelea kuhamasisha vyuo na wadau wa elimu kuwekeza katika programu za sayansi za afya na uhandisi ili kuongeza nafasi za wanafunzi wanaodahiliwa kwenye programu hizo.

Imetolewa na:

Prof. Charles D. Kihampa,
**Katibu Mtendaji,**
Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU)